Kuchunguza Maandiko Matakatifu

Mtihani

Baada ya kusoma na kujifunza somo kwa somo, jibu maswali ya mitihani hii. **Andika jina na anwani yako,** halafu itoe karatasi hii na kuitia katika bahasha. Bandika stempu za kutosha na tutumie kwa anwani ya Shule yetu ya Biblia.

Jina Lako Kamili: _____

Anwani Yako: _____

Kijiji: _____

S.L.P. _____

Mji wa Post Office: _____

Kazi Yako: _____ **Umri Wako:** _____

Maksi ulizopata kwa somo hili ……..%

MTIHANI WA 1. (wa somo la 1.)

Upande wa kulia andika jibu lililo sahihi.

1.. Jumla ya vitabu vya Agano la Kale ni vingapi? _____
2. Kitabu cha kwanza katika Biblia ni kipi? _____
3. Vitabu kuanzia Ayubu mpaka Wimbo wa Sulemani vimejaa nini? _____
4. Kitabu gani cha Biblia kimeandikwa juu ya Makanisa ya kwanza? _____
5. Kuna nyaraka ngapi? _____

Upande wa kulia andika **NDIYO** au **SIYO**.

6. Roho Mtakatifu ndiye aliyesema: "Maandiko hayawezi kutanguka?" _____
7. Tuyafuate Maandiko kama Yesu alivyofanya. _____
8. Agano Jipya lina vitabu 29. _____
9. Injili hueleza juu ya maisha, kufa, kufufuka, na kupaa kwa Bwana Yesu _____
10. Ufunuo hutoa mafundisho yenye shuhuda za maisha ya Kikristo _____

MTIHANI WA 2. (wa somo la 2.)

Upande wa kulia andika jibu lililo sahihi.

1. Utatu wa Mungu una nafsi ngapi? _____
2. Nani hutajwa wa kwanza katika utatu? _____
3. Mungu Baba ni Roho, Mwanadamu au malaika? _____
4. Ni nani aliyeomba: ".... kwani kuna Mungu gani mbinguni au duniani awezaye kufanya mfano wa kazi zako"? _____
5. Mungu Baba na Mwana ni nafsi mbili za utatu, nafsi ya tatu ni nani? _____

Upande wa kulia andika **NDIYO** au **SIYO**.

6. Maandiko huhakikisha kuweko kwa Mungu. _____
7. Wapo miungu watatu. _____
8. Tunaweza kumwabudu Mungu ye yote kama tunavyopenda _____
9. Mungu ana mpango kwa ulimwengu, na wanadamu wote _____
10. Yesu Kristo ni kipawa cha Mungu kwa wanadamu kipitacho vipawa vyote _____

MTIHANI WA 3.(wa somo la 3.)

Upande wa kulia andika jibu lililo sahihi.

1. Yesu huitwa "Imanueli". Maana yake nini? _____
2. Kabla Yesu hajazaliwa alikuwa wapi? _____
3. Nani alikuwa mama mzazi wa Yesu? _____
4. Habari kuu juu ya Yesu inahusu nini? _____
5. Yesu alihukumiwa hukumu gani? _____

Upande wa kulia andika **NDIYO** au **SIYO**.

6. Yesu Kristo ni Mungu. _____
7. Yesu - kama watu wengine - alitenda dhambi. _____
8. Yesu alijeruhiwa kwa makosa yetu. _____
9. Mungu Baba huuonya ulimwengu juu ya dhambi, utakaso, na hukumu. _____
10. Roho Mtakatifu huwajaza Wakristo nguvu ili waishi katika hali ya kumpendeza Mungu_____

MTIHANI WA 4. (wa somo la 4.)

Upande wa kulia andika jibu lililo sahihi.

1. Ni nani aliyemwumba mwanadamu? _____
2. Nani alikuwa mtu wa kwanza? _____
3. Mwanadamu aliumbwa kwa kusudi gani? _____
4. Andika kitabu, sura na mstari usemao: "wote wamefanya dhambi" _____
5. Watu, ambao hawataokolewa watakwenda wapi? _____

Upande wa kulia andika **NDIYO** au **SIYO**.

6. Watu waliumbwa kabla ulimwengu haujaumbwa. _____
7. Dhambi ya kwanza iliyofanywa na Hawa na Adamu ilikuwa ni kutokumtii Mungu. _____
8. Mawazo mabaya si dhambi. _____
9. Hukumu juu ya dhambi, ambayo ni mauti, ni kule kutengwa na Mungu kiroho. _____
10. Mauti hiyo itakuwa ya milele. _____

MTIHANI WA 5. (wa somo la 5.)

Upande wa kulia andika jibu lililo sahihi

1. Wokovu upi ni wa muhimu zaidi - wa kitaifa, wa kimwili, au wa kiroho? _____
2. Nani aliokolewa kutoka katika utumwa wa Misri? _____
3. Andika kitabu, sura, na mstari usemao kuwa wokovu ni kipawa cha Mungu. _____
4. Wokovu hupatikana kwa njia ya nani? _____
5. Nini maana ya neno "Injili"? _____

Upande wa kulia andika **NDIYO** au **SIYO**.

6. Wokovu hupatikana kwa sababu Yesu alikufa msalabani. _____
7. Wokovu haupatikani kutoka kwenye kanisa au ubatizo. _____
8. Ni watu wenye elimu ya juu tu ndio wanaoweza kuokolewa. _____
9. Watu wanaweza kujipatia wokovu kwa kazi zao. _____
10. Ili tuokoke ni lazima tutubu dhambi zetu kwa Yesu na kumpokea kwa imani kuwa Mwokozi na Bwana. _____

Mtihani wa 6. (wa somo la 6.)

Upande wa kulia andika jibu lililo sahihi.

1. Tukisali, kwa kawaida tuombe kwa nani? _____
2. Tuombe kwa jina la nani? _____
3. Nani alisema: "Hatuachi kufanya maombi kwa ajili yenu"? _____
4. Neno la Mungu hutupatia nini? _____
5. Waungwana wa Beroya walifanya nini kila siku? _____

Upande wa kulia andika **NDIYO** au **SIYO**.

6. Katika Biblia kuna mifano mingi ya watu walioomba kwa Roho Mtakatifu _____
7. Yesu alipoomba hakuenda faraghani _____
8. Hatuhitaji kujitenga tunapotaka kuongea na Mungu. _____
9. Kusoma Biblia ni muhimu kwa maisha na kazi ya Kikristo. _____
10. Kujifunza Biblia ni sawa, kuyafuata yote si lazima. _____

MTIHANI WA 7. (wa somo la 7.)

Upande wa kulia andika jibu lililo sahihi.

1. Mkuu wa kanisa ni nani? _____
2. Yesu kabla ya kupaa kwake aliwapa wanafunzi wake agizo gani?

_____

3. Nani aliyepaswa kuwajilia wafuasi wa Yesu ili wapate nguvu?

_____

4. Kanisa ni la baadhi ya waamini, au ni la waamini wote ulimwenguni?

_____

5. Injili ihubiriwe mpaka wapi ? (Matendo 1:8) _____

Upande wa kulia andika **NDIYO** au **SIYO**.

6. Kanisa la sehemu fulani ni mahali ambapo huduma za Kikristo zinafanyika. _____
7. Wakristo wa eneo fulani wakusanyike pamoja. _____
8. Haifai kufanya urafiki na Waamini wengine. _____
9. Kushuhudia majumbani, mashuleni na makazini ni kazi ya Wachungaji tu. _____
10. Kila Mkristo ashiriki katika kanisa linalokubali wokovu. _____

TANGAZO

Ukimfahamu mtu yeyote anayependa kusoma masomo ya Emmaus umwambie kwamba somo la kwanza ni bure. Utuandikie anwani yake.

Rudisha karatasi hii ya mtihani kwetu:
Emmaus Shule ya Biblia,
kwa Njia ya Posta
S.L.P.1424, Dodoma
Tanzania